




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Yah: UHUISHAJI WA LESENI ZA TAALUMA KWA W AUGUZI  
NA WAKUNGA

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda Umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga Nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga inayoitwa "**The Nursing and Midwifery Act, 2010 and its regulations**" **kifungu cha 21 na 38(1)** cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 kinaelekeza kila Mtaaluma kuwa na Leseni.

Zoezi la uhuishaji wa Leseni za Uuguzi na Ukunga kwa msimu wa mwaka **2022/2025** lilianza mnamo tarehe **01/07/2022** na kukamilika tarehe **31/12/2022** kwa gharama za kawaida bila faini. Imebainika kuwepo kwa baadhi ya Wauguzi na Wakunga ambao bado hawajahuisha Leseni.

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga wote kuwa, kuanzia tarehe **01 Julai, 2023** faini za ada za uhuishaji wa Leseni zitaongezeka kwa asilimia **100%** kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Ofisi ya Msajili inaagiza kwa wale wote ambao bado hawajahuisha Leseni kukamilisha kwa kuzingatia utaratibu kwa kuwa ni takwa la kisheria. Aidha, ufuutiliaji utafanyika na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote watakaokiuka agizo hili.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:

Happy Maseenga  
Kny: MSAJILI  
20 Juni, 2023